

Pambazuko

Toleo Namba 053

Jumatatu Novemba 13-19, 2023



Jicho la Tai
Upele CCM
wapata
mkunaji
Uk. 5

Uk. 8

Rais Samia ashangaa wanaomkana Magufuli

- **Makonda adai watu wengi wanafiki**

Tahariri:

Wahariri watathmini ukubwa wao

Uk. 2

Hadhari walaji nyama ya kuku



Uk. 12



Changia uhai wa Pambazuko

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Wahariri watathmini ukubwa wao

MKUTANO Mkuu wa Jukwaa la Wahariri (TEF) unaanza leo katika Mji wa Lindi, ambapo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa Kassim ametajwa kuwa mgeni rasmi.

Takribani wahariri 100 wa vyombo mbalimbali vya habari nchini Tanzania wanajumuika, pamoja na mambo mengine; kujadili mustakabali wao na nafasi ya mchango wa tasnia hiyo muhimu katika ustawi wa fursa, maendeleo, na amani kwa nchi hiyo.

Kaulimbiu ya mkutano huo muhimu ni; “Uandishi wa habari, gesi na uchumi endelevu.”

Ikitazamwa kwa jicho la uchambuzi, kaulimbiu hiyo imechukua kapu-jumuishi ambamo ndani yake kuna taswira ya kuhimiza Watanania kunufaika kwa rasilimali zao; tena bila chembe ya ubaguzi wa maeneo yenye fursa zaidi ya mengine yasiyokuwa nazo.

Ifahamike kwamba, mara zote, vyombo vya habari vimekuwa mhimili usiokuwa na dhamana ndani ya Katiba ya Tanzania, lakini umuhimu wake unaweza kuchukua nafasi sawa ama kuzidi – kwa kiasi, mhimili rasmi; Bunge, Serikali na Mahakama.

Kwamba umuhimu wa vyombo vya habari ni mkubwa mno, kiasi kwamba baadhi ya viongozi waliotukuka, akiwamo Rais wa Tatu wa Marekani, Thomas Jefferson, aliwahi kueleza bila kumung'unya maneno kwamba ikiwa ataambiwa achagoe kuondoa kimoja kati ya vyombo vya habari na serikali katika kuongoza umma, alichagua kubaki kwa vyombo vya habari.

Ni kutokana na umuhimu huo, nafasi ya viongozi wa vyombo hivyo

– wahariri, wanapokutana kujadili mambo yao, wasisahau kuweka msisitizo katika kutumikia umma kwa weledi na uwazi.

Watanania wengi bado wana imani na wahariri na wanabeba mtazamo kwamba ndiyo tasnia iliyobaki kuwapigania kwa kupaza sauti zao pale wanapoona wanaonewa, wanakwamishwa ama wanakandamizwa na wale wenye mamlaka.

Pambazuko linawataкия wahariri wote mkutano mkuu mwema huko Lindi na kwamba katika kujadiliana kwao, wapate fursa ya kupima mchango wa tasnia yao kwa mwaka mmoja katika kupigania haki, neema na fursa kwa Watanania.

Ikiwa vyombo vilifanya vyema, basi wahariri wajipongeze na endapo kuna mahali walikwama, wapate nafasi ya kujirekebisha na kupanga kufanya vyema zaidi miaka mingi ijayo.

Sisi tunatambua kwamba majukumu ya vyombo vya habari, yanazidi kazi za kutoa taarifa tu kwa umma tu na kuwasiliana, lakini pia wahariri wana nafasi ya kutoa mtazamo – kwa niaba ya wananchi kwa kila tukio linalofanyika nchini na hata nje ya mipaka ya Tanzania kwa lengo lilelile la kuona nchi ikineemeka.

Jambo jingine muhimu wakati wahariri wanakutana, ni vyema wakajadili na kupata suluhisho la kujinasua kutoka kwenye lindi la uchumi usioridhisha wa vyumba vya habari na hata mwandishi mmoja mmoja.

Tunawataкия mkutano mwema wahariri wa Tanzania wanapokutana kutathmini ukubwa wao.

MADAKTARI WANGU ASANTENI...



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu (@TunduALissu), wa pili kutoka kulia)- Ijumaa, Novemba 10, alipata wasaa kutembelea Hospital ya Nairobi, Kenya. Madaktari na wauguzi wa hospitali hiyo walishiriki kuokoa uhai wake baada ya kushambuliwa kwa risasi, akiwa Dodoma, Tanzania, Septemba 7, 2017. (Picha kutoka mtandao wa X wa Vitus Nkuna).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Unapoona wenzako wanafanikiwa, acha chuki dhidi yao, kikubwa waombe waendeleo kuwa na heri kwani siku moja, huenda neema zao zikakugusa wewe ama baadhi ya ndugu zako - kwa njia moja ama nyingine - Msemo wa Wahindu.

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandali: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu




Lipa kwa kusan

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI







Upele CCM wapata mkunaji

Na Igo AI

BAADA ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumteua Paul Christian Makonda kuwa katibu wake wa itikadi, uenezi na mafunzo, Tai akaamua kujipa kazi ya kutathmini kazi na mchango wa makada wa chama hicho tawala waliowahi kushika dhamana hiyo.

Tai hakupenda kuanzia mbali, kwani kazi hii hakutumwa na mtu, wala chama hicho hakikumpa kandarasi ya kukifanyia tathmini ya utendaji wa makada wake ili kujua nani hasa anakubalika kwa wanachama na mashabiki.

Basi bhana, Tai akajifungia ndani mahala, akaanza kuvuta faili moja baada ya jingine, ili kwamba apate tathmini sahihi ya utendaji kwa waliopata kuwa makatibu wa itikadi wa itikadi, uenezi na mafunzo wa CCM.

Tai akashika faili la Humphrey Polepole, akalipitia, akachambua – kwa kufungua kurasa moja ya karatasi hadi nyingine, akamaliza faili la kwanza, akaendelea jingine; la pili, la tatu, la nne hadi la tano.

Akashika faili la sita na akafika la saba. Akasoma na kusoma. Akaweka pembeni mafaili ya Polepole na kuanza kuandika tathmini yake.

Tai akabaini kuwa kidogo hapo CCM ilipatia, ingawa shida moja, kada huyo alikuwa anafanya mbwembwe nyingi, zingine za kitotototo katika kukitangaza na kukikuza chama hicho.

Kutokana na wingi wa mafaili ya Polepole. Tai akajipa breki kidogo, jioni akasogea jirani na baa moja akapoza koo kutokana na mavumbi kutoka kwenye mafaili aliyokumbana nayo wakati wa kazi yake.

Kesho yake, Tai akashika mafaili ya Sophia Edward Mjema; akapekua faili la kwanza, akaenda la pili na akashika la tatu na hapo mchezo wa kuyapitia



*Katibu wa itikadi, uenezi wa CCM,
Paul Makonda*

ukaisha, Haikuwa kazi ngumu maana mafaili yenyewe, mengine yana karatasi moja ama mbili.

Tai akabaini, ndani ya mafaili yale, hakuna cha kutathmini kwani yalijaa barua za kupongeza, kufurahia na kuzodoana hapa na pale na baadhi ya watendaji wa chama hicho. Tai akafunga ofisi na kwenda kuzurura.

Siku iliyofuata, Tai akapiga moyo konde, kwamba huenda akakutana na mafaili mengi sana ya Paul Makonda.

Kweli bhana, kama alivyotea, kuitisha mafaili ya Makonda, akaletewa mlima wa makabrasha licha ya kuwa na siku chache ndani ya ofisi, hata hivyo, hakuogopa, kwani “maji ukivyavulia nguo...”

Tai akaanza na faili la kwanza; masalaalee! Akakutana na nyaraka zenye kubeba amri, nguvu ya mamlaka, zikielekeza hili ama lile kwa mawaziri wa serikali.

Akashika faili la pili, akakutana na karatasi kibao zinaelekeza Makonda aandaliwe farasi, sijui pikipiki, sijui bajaji, sijui watu kumbeba mgongoni, atakapoanza ziara zake. Mambo ni mengi!

Tai akafunga kazi na hakuendelea tena na kazi ya tathmini aliyojitwika. Akaondoka huku akijisemea; “ama kweli upele wa CCM umepata mkunaji.”

Habari

SGR kupata umeme wa uhakika

Na Mwandishi WETU

SERIKALI ya Tanzania “imejipiga kifua”- kwa umma kwamba sasa ipo tayari kuhudumia reli na treni ya mwendokasi (SGR)kwani umeme wa uhakika upo.

Jitihada za kuwepo kwa umeme wa uhakika, zinathibitishwa na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kushuhudia hatua mwisho za maendeleo ya kukamilisha miundombinu ya nguvu hizo za nishati kuendesha usafiri huo unaosubiriwa “kwa hamu na gamu” na Watanania.

Kutokana na hatua hizo zilizofikiwa, ni kama Tanesco wanasema; “sasa treni ya mwendokasi ije.”

Katika ziara yake kwene mitambo ya kupatikana kwa umeme wa uhakika, Kamati hiyo ya Bunge imeona utayari wa miundombinu ya umeme kwa ajili ya reli na treni ya mwendokasi mkoani Morogoro.

Akizungumza katika ziara hiyo iliyofanyika hizi karibuni, mwenyekiti wa kamati hiyo, Dkt. Mathayo David Mathayo ameipongeza serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umeme kwa ajili ya reli na treni ya mwendokasi kutoka Kinyerezi, Dar es Salaam mpaka Kintiku, Singida.

“Tumelezwa mradi wa ujenzi miundombinu ya umeme kwa ajili ya uendesaji reli na treni ya mwendokasi kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro umekamilika kwa asilimia 100,” ameongeza Dkt. Mathayo.

Dkt. Mathayo ameeleza kufurahishwa

na jitihada za Tanesco kuhakikisha kwamba umeme hauwezi kuwa kikwazo katika kupatikana kwa maendeleo ya nchi na watu wake.

“Sisi kamati tumeridhishwa sana na uwekezaji ambao serikali imeufanya na juhudi za wenzetu wa Tanesco katika kupata umeme wa uhakika,” amongeza Dkt. Mathayo.

Tanesco inaeleza kwamba mradi wa kutoa umeme Morogoro kupeleka Kintiku umefikia asilimia 99.

Dkt. Mathayo amehimiza Wizara ya Nishati kupitia Tanesco kuongeza usimamizi ili kuhakikisha asilimia moja iliyobakia ya ujenzi wa miundombinu ya umeme inakamilika mapema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga amehakikishia kamati kuwa wizara anayoongoza, itaendelea kusimamia miradi ya miundombinu hiyo ya umeme ili inapoanza kazi, usafiri huo wa uhakika usikwame.

Katika hatua nyingine naibu waziri huyo amemuagiza mkandarasi Xian XD Electrical Engendering, anayetekeleza ujenzi wa upanuzi wa kituo cha kupoza na kupokea umeme cha Msamvu, Morogoro kukamilisha ujenzi huo kufikia Disemba 3, mwaka huu ili kuboresha zaidi kupatikana kwa umeme wa uhakika mkoani Morogoro.

Tanzania iliazimia kujenga reli ya kisasa – na yenye mwendokasi - usiopungua kilometa 160 kwa saa, lengo likiwa ni kuenza mtandao usiopungua kilometa 2,561 ikiunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Katavi na nchi zinazokuwa na bandari (Rwanda, Burundi, DRC).



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dkt. Mathayo David Mathayo akiwa na baadhi ya wajumbe wenzake alipokagua mitambo ya umeme eneo la Msamvu, Morogoro.

Matajiri zaidi Afrika, Tanzania imo

Na Scovy MANASE

TANZANIA inatajwa kushika nafasi ya 10 kwenye orodha ya wafanyabiashara wenye ukwasi zaidi katika Bara la Afrika.

Ukwasi unaotajwa ni kwa matajiri wanaofikia ama kukaribia dola bilioni moja za Marekani.

Katika Tanzania, matajiri wakubwa wanaotajwa – wote wakiwa na nasaba za Bara Asia, ni pamoja na Mohammed Dewji (MO), Said Salim Bakhresa, Rostam Aziz, Ally Awadh, Shekhar Kanabar, Ghalib Said Mohammed (GSM) na Yogesh Manek.

Katika taarifa iliyopatikana jana, inaeleza kuwa zaidi ya asilimia 90 ya mabilionea walioko Afrika, wako katika mataifa matano; Afrika Kusini, Misri, Nigeria, Kenya, na Morocco.

Mabilionea katika nchi hizo wanatajwa kwa pamoja, kuchangia asilimia 56 ya watu wenye utajiri mkubwa wa fedha na mali Afrika.

Afrika Kusini ndio taifa lenye matajiri wengi zaidi katika bara hilo, huku miji yake minne kati ya miji 10 ya utajiri zaidi



Mo

barani Afrika, ikipatikana nchini humo. Jiji la Johannesburg ndilo jiji lenye mabilionea wengi Afrika ikiwa na mamilionea 14,600.

Kulingana na takwimu za karibuni za New World Wealth, kuna takriban nyumba za kifahari 3,700 nchini Afrika Kusini ambazo zina thamani kubwa zaidi, zikipiku nyumba nyingi katika majiji makubwa ya Marekani.

Sambamba na takwimu hizo, pia inaelezwa kuwa Afrika Kusini ni moja ya masoko 20 makubwa ya nyumba



Bakhresa

za makazi na kifahari duniani, ikiwa inatanguliwa na nchi nyingine za Ulaya, Asia na Marekani.

Misri inashika nafasi ya pili ikiwa na idadi ya mamilionea wengi barani Afrika.

Kenya ndio nchi ya nne yenye matajiri ikiwa na mamilionea wanafikia 7,700.

Idadi ya mamilionea barani Afrika inatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 42% katika kipindi cha miaka 10 ijayo, na kufikia karibu 195,000 ifikapo 2032, kulingana na ripoti hiyo.

Katika hatua nyingine, jarida la World of Statistics la hivi karibuni, limetoa orodha ya watu matajiri zaidi duniani – wenye ukwasi wa mabilioni ya dola za Marekani, huku Elon Musk akiwa “ametupwa” kwenye rekodi ya kuwa mtu tajiri zaidi duniani.

Nafasi hiyo sasa inashikiwa na Bernard Arnault, mfanyabiashara mkubwa kutoka nchini Ufaransa, akiwa amewekeza zaidi kwenye sekta za sanaa. Yeye ndiye mwanzilishi, mwenyekiti, na afisa mkuu mtendaji wa LVMH Moët Hennessy, Louis Vuitton, kampuni kubwa zaidi ya bidhaa za anasa (luxury) duniani. Utajiri wake unakadiriwa kuwa ni dola bilioni 190.

Musk anashika nafasi ya pili, akiwa ni mfanyabiashara mkubwa na mwekezaji mzaliwa wa Afrika Kusini kwa sasa akiishi nchini Marekani.

Yeye ndiye mwanzilishi, mkurugenzi mtendaji na mhandisi mkuu wa SpaceX, mmiliki wa mtandao wa X (zamani Twitter). Utajiri wake unakadiriwa kuwa ni dola bilioni 146.

Habari

Rais Samia ashangaa wanaomkana Magufuli

Na Mwandishi WETU

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda amebainisha kwamba Rais Samia Suluhu Hassan, anawashangaa wanaombeza na kumkana mtangulizi wake, John Pombe Magufuli.

Makonda amesema Rais Samia anawatambua wote wanaombeza Magufuli na kuamini kuwa ipo siku watambeza na kumkana hata yeye; akiwa madarakani ama baada ya dhamana hiyo.

Jana, akiwa njiani kuelekea Mwanza kuendelea na ziara yake Kanda ya Ziwa, Makonda alipata fursa ya kuzungumza na wananchi wa Mji wa Sengerema na kueleza namna baadhi ya watu kuwa wanafiki kwa kumsifia mtu anapokuwa madarani au kuwa na mali.

Makonda akadai, Rais Samia amekuwa akiangalia namna watu wanavyobeza mchango wa magufuli wakati wa uongozi wake, bila kujali mambo makubwa aliyofanyia Tanzania na watu wake.

Rais Samia alipokea kijiti cha uongozi wa nchi kufuatia kifo cha Magufuli kilichotokea Jumatatu, Machi 17, 2021. Samia aliipishwa kuwa Rais wa Tanzania baada ya siku mbili.

Katibu huyo mwenye kazi ya kupaza sauti ya kukitangaza chama chake, akadai kuwepo kwa watu wanafiki ambao kazi yao kubwa ni kijipendekeza na kuchungulia fursa kupitia kwa watu wenye madaraka ama neema za kiuchumi, kwa manufaa binafsi.

“Rais Samia ni mama mwenye hekima na busara kubwa mno, anatumia sana akili na anawaangalia tu mnaomkana hayati Magufuli, anajua ipo siku mtamkana na yeye kwa hiyo kuweni na upendo wa kweli, chama cha mapinduzi kimetulea na kutufunza, naamini hatujafunzwa kuwa wanafiki,” ameoongea.

Makonda amekemea watu kwa kukosa



Samia akiapa kuwa Rais wa Tanzania

shukrani na kushindwa kutoa michango ya heri kwa watu “waliowashika mkono” wakati wa shida ama dhamna za maisha.

“Mimi ni muumini wa kutambua chanzo cha baraka, kama hutambui chanzo chako cha baraka zako zimeanzia wapi, basi hata atakayekupa baraka kwa sasa, bado hutomshukuru, ni vyema kushukuru na kutambua baraka ulizopewa,” ameoongea.

Katibu huyo wa uenezi akawageukia waniasia kwa kuwaeleza kwamba ni wepesi wa kusahau mema wanayofanyiwa na watu wengine na kwamba ni wakati sasa wa kutambua mema wanayotendewa na ikibidi watoe shukrani za dharti.

“Waniasia wenzangu niwaambie tu ukweli, msisahau watu waliowashika mikono, wapo watu wanamsema vibaya Hayati Magufuli na kusahau mema aliyowatendea na watu kama hao maana yake siku moja watakuja kusahau mema hata wanayotendewa na Rais Samia,” akasema Makonda.

Baada ya kutangazwa kushika wadhifa huo ndani ya chama hicho tawala, Makonda alianza ziara mikoani ambako anapita na kufanya mikutano ya ndani na hadhara, huku baadhi ya watendaji wa serikali, wakiwamo mawaziri, wakiongozana naye.



Mkurugenzi Korosho amepotoshwa au nini?

Na Rashid Mtagaluka

KAULI aliyoitoa Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Alfred Francis wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wiki iliyopita kuhusu bei ya korosho minadani, haiwezi kuachwa bila kujadiliwa.

Katika mkutano huo wa Oktoba 30, 2023, Francis alikuwa anajaribu kujibu hoja za viongozi wa ACT-Wazalendo waliopendekeza serikali ichukuwe hatua mbalimbali kusaaidia wakulima wa korosho, ikiwa ni pamoja na kupunguzwa kwa tozo zinazowaongezea mzigo wakulima hao.

Jambo la kushangaza, mkurugenzi huyo badala ya kwenda kujibu hoja hizo na nyingine, aliamua kufanya propaganda ninazoamini kuwa hazina tija kwa wakulima wa korosho.

Alisema kwamba tangu kuanza minada hiyo Oktoba 20, mwaka huu, bei ya chini ya korosho ilikuwa Sh.1,900 huku bei ya juu ikiwa Sh.2,900 - ikilinganishwa na mwaka uliopita, huku akisisitiza korosho ni zao linalozalishwa na nchi 35 na bei zao ziko chini.

Kama kuna mahala mkurugenzi huo aliteleza ni pale alipotolea mifano nchi mbalimbali ikiwemo Msumbiji ambayo alidai msimu wa kuuza zao hilo unalingana na Tanzania, lakini wao bei elekezi waliweka sh. 1,350 kwa kilo moja.

Akadai Nigeria bei yao ni sh. 1450, Bukinafaso sh. 1050 kwa kilo, kwa hiyo ukiangalia bei za wenzetu wameuza korosho ghafi kwenye masoko yao, Tanzania utaona tuko juu kuliko wenzetu.

Hebu tuiangalie Msumbiji, tuachane na Nigeria na kwingineko, alikokutaja ili tuone maelezo aliyoyatoa yalilenga kutatua changamoto ya mkulima wa korosho ama yamelenga vitu vingine



Zao la korosho

kabisa.

Ni kweli bei ya chini ya korosho katika minada iliyofanywa na vyama vikuu vya Tanecu, Mamcu, Lindi Mwambao, pamoja na Runali ilikuwa ni sh.1,900.

Hata hivyo, hakuna mahala popote mpaka leo hii ambako bei ya juu ya korosho imenunuliwa Sh. 2,900. Bali bei ya juu ni Sh. 2060/-tu.

Kuhusu propaganda za mkurugenzi huyo kulingana na nafasi ndogo ya ukumbi huu tuitazame sarafu ya Msumbiji inayoitwa Mitikal 1,350 hapa kwetu ni kama Sh.33,000, hivi kweli mkurugenzi wetu hajui au alipitiwa?

Mwaka 1999, kilo moja ya korosho iliuzwa kati ya Sh. 800 hadi 950; ambayo mkulima akiuza kilo moja tu alikuwa anaweza kupata mlo wake wa siku yeye na familia ya watu wanne na chenji ilibakia.

Kumbe kama miaka 24 iliyopita kilo moja ya korosho ilimwezesha Mtanzania anayeishi kijijini – akilima korosho, kupata chakula cha kawaida, korosho ya mwaka huu imepata masahibu gani?

Mwandishi anapatikana kwa simu namba: 0784438546 au Email: mtagaluka@gmail.com

Habari**Barabara njia nne zanukia Mwanza**

Na Tryruckia MFINANGA

KASI ya kukua kwa Jiji la Mwanza kunakwamishwa na ufinyu wa barabara zinazolingia na kutoka, hivyo kudhoofisha maendelo yake.

Hivyo, kunasua mkwamo huo, Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza kujengwa kwa barabara za njia nne kwenye maeneo mengi ili kwenda sambamba na ukuaji wa jiji hilo.

Rais Samia ameelekeza Wizara ya Ujenzi kufanya usanifu wa kina wa barabara za Mwanza Mjini hadi Usagara na barabara ya Mwanza Mjini hadi Igoma ili zipewe kipaumbele katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 kwa ajili ya kujenga barabara za njia nne.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amebainisha hayo jana akiwa Mwanza ambako aliwahakikisha wananchi kuwa Rais Samia ameahidi kukamilisha ujenzi huo haraka.

“Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia amenielekeza kufanya haraka sana usanifu wa kina wa barabara za Mwanza Mjini Kwenda Usagara Kilometa 22 na Mwanza Mjini kuelekea Igoma ili ziwekwe kwenye vipaumbele vya bajeti ya 2024/25 kujengwa kwa njia nne,” amesema Bashungwa.

Bashungwa pia amesema Rais Samia tayari ametoa kibali kwa mwaka huu wa fedha, kujengwa kwa barabara ya kutoka Uwanja wa Ndege wa Mwanza - Igombe hadi Nyanguge, Magu iliyopo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 kwa kuanza kujenga kwa kiwango cha lami kilomita 10.

Waziri huyo sambamba na ujenzi wa barabara, pia ameelekeza kuwa kwa kutambua umuhimu wa Daraja la Magufuli katika kuunganisha ushoroba wa Ziwa Viktoria, unaoanzia Sirari, mpakani mwa nchi ya Tanzania na Kenya hadi Mutukula Mpakani mwa Tanzania na Uganda, barabara hiyo itapanuliwa

**Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa**

na kuwa na njia nne ili kupunguza msongamano wa magari.

“Mwelekeo huu ni sambamba na kukamilika kwa daraja la Magufuli, Ujenzi wa SGR (treni ya mwendokasi), vivuko vinne vipya na vitano vinavyokarabatiwa, haya yote yanaenda kulifanya Jiji la Mwanza kuwa moja ya majiji bora ukanda huu wa Afrika” ameelekeza Bashungwa.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makala, amesema ujenzi wa Daraja la Magufuli una manufaa makubwa na likikamilika, litaokoa muda wa wananchi kusubiri vivuko kwani sasa vinatumia dakika tatu hadi nne kuvuka kwenda upande wa pili wa Busisi.

Akitoa taarifa ya mradi wa ujenzi, Meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroads), Mkoa wa Mwanza, Pascal Ambrose, amesema daraja hilo likikamilika litakuwa daraja la kwanza kwa ukubwa katika nchi za Afrika Mashariki na Kati ambapo pia ni daraja la Sita kwa urefu barani Afrika.

Mbunge wa Sengerema, Hamisi Tabasamu, amesema sambamba na ujenzi wa daraja hilo, Rais Samia ametoa kibali cha ujenzi wa barabara ya Sengerema hadi Irunda.

Athari ya mvua kubwa Dar

Maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam, jana yalikumbwa na mafuriko kufuatia kunyesha mvua kubwa. Maeneo hasa ya mabondeni ndiyo yameathirika zaidi kwa nyumba kujaa maji na kubomoka. Pia kukwamisha usafiri baada ya barabara nyingi kushindwa kupitika kwa kujaa maji ama madaraja kubomolewa. Picha hizi zimechotwa kutoka kwenye mitandao ya kijamii. (Huenda zingine siyo za tukio la mvua za jana).



Kenya

Tahadhari walaji nyama ya kuku

Na Charles WASONGA
Nairobi

SERIKALI ya Kenya imetoa tahadhari kuhusu usalama wa nyama ya kuku inayouzwa katika Jiji la Nairobi na miji mingine mikuu nchini humo.

Mkurugenzi wa Idara ya Afya ya Mifugo, Obadia Njagi amesema jana kuwa nyama nyingi za kuku zinazouzwa katika maduka mengi, hazijakaguliwa na maafisa wa afya.

Njagi anasema kumekuwepo na idadi kubwa ya kuku wanaochinjwa kwenye nyumba za watu, badala ya kufanya hivyo kwenye maeneo maalum; hasa machinjio maalum yaliyoainishwa na sheria za Kenya.

Mkurugenzi huyo pia amelieleza Taifaleo kuwa kuwa usafirishaji nyama ya kuku inayotolewa kutoka kwenye nyumba za watu binafsi na kupelekwa kwenye maduka, unakiuka kanuni za afya zilizowekwa ili kulinda usalama na usafi wa watumiaji.

“Nyama hii hupatikana moja kwa moja kutoka kwa wafugaji wa kuku wa nyama, ambao huwachinja katika vibanda vyao na kuisafirisha hadi kwenye maduka ama kwa wale wenye migahawa na vioski vya kuuza chakula,” amesema na kuongeza – “nyama hii siyo salama.”

Tayari Njagi amewaandikia barua watendaji na wakurugenzi wa idara yake katika ngazi za kaunti ili kuwafahamisha kuanza kuchukua hatua stahiki kunusuru watumiaji wa nyama ya kuku inayouzwa kiholela.

Inaelezwa kuwa maeneo mengi yanayouza kuku wasiokaguliwa ni maeneo yanayouza vyakula vinavyoandaliwa haraka-haraka (fast food) katikati mwa Jiji la Nairobi na miji mingine mikubwa nchini.

Katika hatua nyingine, imethibitika kuwa baadhi ya maeneo maalum ya kuchinjia kuku, yamekuwa yakipokea kuku waliochinjwa majumbani na wao



Nyama ya kuku

kuuza tu, hatua ambayo ni kinyume cha sheria za Kenya.

Hatua hii ni kinyume na Sheria ya Kusimamia Usalama wa Nyama, Kifungu cha 356 inayosema kuwa wanyama wa kuliva sharti wachinjwe katika machinjio yaliyoidhinishwa na kupewa leseni na ambayo hukaguliwa mara kwa mara na maafisa husika.

Njagi amewashauri wakaguzi wa nyama katika kaunti zote kufuatilia kwa makini mwenendo huo mbaya unaoweka afya na hasa maisha ya Wakenya hatarini.

Idara hiyo pia imeonya kuwa wafanyabiashara watakaopatikana na hatia ya kukiuka sheria na mahitaji kuhusu nyama ya kuku sambamba na mifugo mingine, watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Sheria za Kenya zinawataka wafanyabiashara wa nyama ya aina yoyote kununua kutoka maeneo mahsusi na kuhakikisha nyama wanayonunua imepimwa na wataalamu wa afya kabla ya kuwafikishia walaji.

Kuuza nyama yoyote isiyopimwa wala kukaguliwa na wataalamu wa afya, huwaweka wateja katika hatari ya kununua nyama isiyu salama na yenye vimelea vinavyosababsha maradhi.

Mbali na maeneo ya Nairobi, imethibitika pia kuwa biashara za kuchinjia na kuuza nyama za kuku inazidi “kunoga” hata katika maeneo mengi jirani na makazi ya watu.




Tsh. 30,000
Food & Drinks

December
10-2023

10:00am
to
17:00pm

ACTIVITIES

Music & Dance, Art & Craft
Face Painting, Pretend Play
Jumping Castles
Many more fun games



call:0714 521 038
0687 457 561 Address: Greengate Garden

Habari-Picha

Wahariri waongeza kipato Nangurukuru

BAADA ya kusafiri zaidi ya kilomita 290 kutoka Dar es Salaam kuelekea Lindi jana, baadhi ya wahariri waliamua kupumzika na kupata wasaa wa kula chakula eneo la Nangurukuru, Kilwa.

Katika eneo maarufu la kuhudumia wasafiri Nangurukuru, wahariri walinunua vyakula, “waliwaungisha” wajasiriamali kwa bidhaa mbalimbali na zaidi sana walipata muda wa kusikiliza changamoto za wafanyabiashara wa eneo hilo na kuahidi kupaza sauti kwa niaba yao.

Leo wahariri wataanza kikao chao cha Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), huku mgeni rasmi akiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Katika picha hizi, wahariri wanaonekana wakifurahia chakula na wengine kuzungumza na wafanyabiashara. (Picha zote kwa hisani ya TEF).





Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Sudan

Usalama tete, msaada wahitajika

Na Mwandishi WETU

BADO hali ya usalama nchini Sudan, ni tete na maisha ya watu yanazidi kuwa mabaya zaidi, huku misaada ya kibinadamu ikihitajika kuwafikia haraka.

Umoja wa Mataifa (UN) umetoa hadhari hiyo mwishoni mwa wiki baada ya kufanya tathmini na kubaini hatari kubwa inayoweza kutokea kwa watu – kwani “machafuko zaidi yananukia.”

Inataarifiwa kuwa mapigano kati ya majeshi ya serikali ya nchi hiyo na makundi ya wanamgambo, bado yanaendelea na kwamba huenda kila kundi likaongeza nguvu, hivyo kuleta madhara makubwa.

“Kinachotokea sasa kinaelekea kwenye uovu zaidi,” mratibu wa UN kuhusu masuala ya kibinadamu katika taifa hilo la Afrika, Clementine Nkweta-Salami alisema juzi, Ijumaa.

Machafuko ya Sudan yaliibuka kuanzia katikati ya mwezi wa Aprili, mwaka huu wakati mvutano mkali wa kisiasa, kati ya mkuu wa jeshi, Jenerali Abdel-Fattah Burhan na kamanda wa kikosi chenye kujiita cha msaada wa haraka, Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, ulipolipuka na kuwa vita kutoka kwa wafuasi wao.

Clementine aliuambia mkutano wa Umoja wa Mataifa kuwa “hali inatisha na kusikitisha” na kusema ukweli, tunaishiwa maneno ya kuelezea hofu ya kile kinachotokea,” na kulisitiza kuwa “mgogoro wa Sudan bado haujapoa.”

Pamoja na kwamba pande hizo mbili zenye mzozo ziliwahi kuketi huko Jeddah, Saudi Arabia na kutia saini makubaliano ya kuacha mapigano, bado makundi hayo hayaaminiani na hayajaacha vita.

Inaelezwa kuwa zaidi ya watu milioni 25 wanahitaji msaada wa haraka ili kuwaepusha dhidi ya njaa na magonjwa.

Katika kuhakikisha amani inapatikana, Jumatatu iliyopita, UN iliwaalika na



kuwashirikisha viongozi wa makundi hayo kwenye meza ya mazungumzo ili kufikia muafaka wa kuacha vita.

Mkutano wa maofisa wa UN na majenerali wanaopigana walikubaliana kuanzisha Jukwaa la Kibinadamu, ili kuacha mauaji na uharibifu.

Kutokana na vita hivyo, inakdirwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya vituo vya afya katika maeneo yenye migogoro havina huduma, hivyo kuhatarisha uhai wa watu.

Inaelezwa na UN kwamba upo uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa ongezeko la vifo vya watu kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa kipindupindu na homa ya dengue, malaria na surua, hasa katika maeneo ambayo huduma za afya hazipo.

“Tunachokiona ni magonjwa njaa inayoongezeka, karibu kila mahali, hawa watu wanajhitaji msaada wa haraka zaidi,” alisema Clementine.

Clementine amehimiza nchi tajiri na mashirika ya kibinadamu kuharakisha kupeleka misaada ya kibinadamu huko Sudan, ili kunusuru uhai wa watu wanaoteseka kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Sudan imekuwa ikikumbwa na machafuko ya mara kwa mara, na mengi yanatokana na kugombea madaraka.



Ahukumiwa kunyongwa kwa kuua 'hawara' wa mume - 2

SEHEMU ya kwanza ya mfululizo wa simulizi za kesi hii tumeona namna muuaji alivyopanga njama za kuua mwanamke mwenzake, sasa endelea sehemu ya pili:

MTUHUMIWA utetezi wake ulikuwa kwamba, marehemu Happiness alimkashifu kupita kiasi wakati alipokuwa hapo nyumbani kwake, kiasi kwamba alipatwa na hasira kali zilizopitiliza na kumpiga na kipande cha chuma kichwani mara moja.

Katika maelezo yake wakati anahojiwa, Asha alitoa maelezo marefu kuhusiana na maisha yake na matatizo yake ya ndoa na Dkt. Hauli.

Aliendelea kueleza jinsi alivyokuja kugundua kuhusu uhusiano aliyokuwa nao Happiness na mumewe na jinsi alivyokuwa akipelekwa mara kwa mara Polisi na Happiness kujibu tuhuma kwamba alikuwa akimtishia kumdhuru.

Asha alidai kwamba mnamo tarehe 22 Novemba, alikwenda tena Polisi kama alivyoelekezwa, baada ya suala lao kuahirishwa siku moja iliyopita. Alipofika pale alimkuta Happiness tayari ameshafika.

Lakini askari huyo aliwaambia kwamba asingeweza kusikiliza shauri lao kwa sababu Dkt. Hauli hayupo nchini kwa hiyo wasubiri mpaka hapo atakaporudi, ndipo wazungumzie shauri lao na kupatiwa muafaka.

Askari huyo wa upelelezi aliwasihhi wasije wakadhuriana wakati wanamsubiri Dkt. Hauli, baada ya kuwaonya Happiness ndiye aliyekuwa wa kwanza kuondoka hayo kituoni.

Baada ya dakika 10 na yeye aliondoka na alimkuta Happiness akiwa kasimama kwenye taa za kuongozea magari pale Salender Bridge akiwa anasubiri kuvuka.



Asha Mkwizu akiwa amefunika uso baada ya kutoka kusikiliza hukumu yake.

Walivuka pamoja upande wa pili ilipo Hoteli ya Palm Beach. Ndipo Asha alipomuaga Happiness na kumtaka amfikishie salaam zake kwa mkuu wa shule anakofanyia kazi yeye Happiness.

Lakini Happiness akadai kwamba haendi shule moja kwa moja. Lakini pia akamwambia Asha kwamba anajisikia njaa na anahitaji kitu cha kula.

Asha alimweleza kwamba kwa muda ule hakuna huduma pale katika Hoteli ya Palm Beach, kwani ilikuwa ni saa nne asubuhi.

Happiness alimuuliza ni wapi anaweza kupata duka la vinywaji baridi na ndipo Asha akamjibu kuwa jirani na anapoishi kuna kioski kinauza vinywaji baridi na kuku wa kukaanga.

Happiness alisema ni vyema akioneshwa hicho kioski. Walikubaliana waende pamoja ili baadaye yeye Happiness awahi kwa dada yake ambaye ilikuwa ampeleke kwa Dkt. Mvungi kwa matibabu.

Kwa maelezo hayo Asha alionekana

Kesi Zilizosisimua



Ahukumiwa kunyongwa kwa kuaa 'hawara' wa mume - 2

Inatoka Uk. 17

kukwepa hoja kumshawishi Happiness ili wafuatane nyumbani kwake kama alivyonukuliwa katika maelezo ya awali wakati akihojiwa na askari wa upelelezi.

Asha alidai kwamba hakuwa katika hali nzuri wakati anahojiwa na askari wa upelelezi, Alfred Gewe na hakusomewa maelezo yake na badala yake alitakiwa kuweka sahihi katika sehemu zote zilizowekwa alama X.

Asha aliendelea kueleza kwamba walifika jirani na kioski alichomweleza, na akamkaribisha nyumbani na akakubali.

Walipofika nyumbani, Asha alitoka kwenda kununua chupa mbili za bia na chupa moja cocacola. Alichanganya bia na cocacola kwenye glasi akiwa jikoni kwa sababu Happiness alitaka achanganyiwe vivywaji hivyo kwa mtindo huo.

Walikunywa pamoja vinywaji hivyo pamoja na kula ndizi. Wakati huo walikuwa wakizungumza pamoja.

Asha alimweleza Happiness ni kwa jinsi gani wote wawili walivyo na mnasaba na Dkt. Mvungi. Na hapo ndipo Happiness aliposema Dkt. Hauli ni wake na hawezi kumwacha mpaka kufa.

Baadaye aliomba aonyeshwe kilipo choo, ambapo alionyeshwa.

Akadai kwamba Happiness aliporejea ndani, alimkuta Asha anaosha glasi hapo jikoni, Happiness alifika hapo jikoni na wakati ananawa mikono yake akaanza kumkashifu.

Happiness akadaiwa kwamba alisema; "hivi kwa nini unanifuata fuata wewe kizee, huna thamani tena na umeshakwisha, na u mgumba. Kama mumeo angekuwa anakuthamini angekufungia wewe na wanao kuja kupitisha usiku kwangu?"

Asha akamwambia, "Happiness, wewe ni kama mwanangu, huwezi

kunitusi kiasi hicho." Ndipo Happiness akamwambia Asha kwa kipare, "Chebakie ni Kushoshorwa hena mzuri na vichaa." (mahakama ilitafsiriwa maneno haya – Pambazuko haliwezi kuyaweka hapa.

Na baada ya kusema hivyo ikadaiwa kwamba Happiness alimsukuma Asha na kudondokewa na shubaka mguuni, na kwamba wakati Asha anaondoa shubaka lile mguuni mwake, Happiness alimfuata pale alipo na ndipo alipookota kipande cha chuma na kumpiga nacho.

Kwamba baada ya kitendo kile, aliona damu nyingi ikivuja kutoka kichwani kwa Happiness na alijaribu kumpa huduma ya kwanza lakini haikuwezekana, Happiness Alifariki.

Kuhusu kuuchoma moto mwili wa marehemu kabla ya kuuzika, mtuhumiwa alidai kwamba tukio hilo lilitokea kama bahati mbaya.

Mtuhumiwa alikanusha kumwambia kijana wake wa kazi Musa kuwa asirudi nyumbani mpaka saa sita mchana.

Akadai anakumbuka kumweleza Musa kwamba awe makini asije akakamatwa na Polisi kama mzururaji kwa sababu hakuwa na kitambulisho.

Pia alikanusha madai ya Musa aliyowaeleza Polisi kwamba yeye Asha alichimba shimo kwenye bustani kabla ya kumuua Happiness.

Madai mengine aliyokanusha ni kuhusu kumweleza Musa kwamba amemua adui yake.

Alisema alimweleza Musa kwamba kuna tukio limetokea kwa bahati mbaya na amemua mtu na kumzika katika bustani na alimuonesha Musa kaburi alipomzikia Happiness.

Asha alieleza mahakama kwamba kama angekuwa na dhamira ya kumuua Happiness, basi angemua kwa sumu

Itaendelea toleo lijalo...

Robertinho aponda usajili Simba

Na Mwandishi WETU

UONGOZI wa Timu ya Soka ya Simba iliamua “kumtoa kafara” kocha Roberto Oliveira ‘Robertinho’- kuficha aibu ya kufungwa na watani wao, Yanga.

Wiki iliyopita; Novemba 5, mabingwa watetezi, Yanga waliwaadhibu watani wa jadi, Simba kwa kuwatandika mabao 5-1 katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Benjamín Mkapa Jijini Dar es Salaam.

Baada ya kipigo hicho, Simba ilimtimua kocha wao ikiwa ni njia ya ‘kufunika aibu’ kwa wapenzi na mashabiki wao.

Hatua hiyo ilikuwa ni njia kuonesha dunia kwamba huenda Robertinho hajafikia viwango vinavotakiwa na timu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Dar es Salaam.

Hata hivyo, katika kuweka kumbukumbu sawa na kulinda hadhi yake, kocha huyo amejitetea kwa kueleza kuwa kipigo cha Simba kutoka kwa Yanga ilikuwa halali kwa kuwa “viwango vya wachezaji wengi Simba, bado butu.”

Akizungumza wiki iliyopita na Kitenge Sports, Robertinho alisema Simba ilikosa kusajili wachezaji bora zaidi katika dirisha lililopita.

Robertinho amedai kuwa usajili wa Simba haukuwa na tija kutokana na idadi kubwa ya wachezaji kukosa ubora wa kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza.

Mbrazil huyo amebainisha kuwa kati ya wachezaji 11 waliosajiliwa na timu hiyo katika dirisha lililopita, ni wawili tu ambao wanaweza kushindania nafasi kwenye kikosi cha kwanza ambao ni beki Che Fondoh Malone na kiungo Fabrice Ngoma.

“Hakuna njia ya mkato kwenye



Kocha Roberto Oliveira 'Robertinho'.

kutafuta mafanikio kupata timu bora, huwezi kuijenga kwa kutumia dirisha moja la usajili, sikiliza kwenye usajili uliopita tuliwaleta wachezaji wengi, lakini ni wawili tu wanaweza kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza...

... Jambo zuri ambalo Simba itajivunia, tulibakiza baadhi ya wachezaji ambao walikuwa msingi wa timu ambao walipoungana na wengine, tukajaribu kuwa na timu yenye upinzani,” alisema Robertinho.

Wachezaji 11 waliosajiliwa na Simba katika dirisha lililopita la usajili ni Fabrice Ngoma, Che Malone, Hussein Kazi, Ayoub Lakred, Aubin Kramo, Luis Miquissone, Shaban Chilunda, Hussein Abel, David Kameta, Willy Onana na Hamisi Abdallah.

Mashabiki na wapenzi wengi wa Simba wamekuwa wakiulaumu uongozi wao kwa “kutapatapa” baada ya kufungwa na Yanga na wanashauri kwamba ni bora kujipanga kwa usajili mpya mzuri, badala ya kulaumiana, kufukuzana ama “kushikana uchawi.”



Moja ya picha ya ubunifu iliyowasilishwa na Mariola Glajcar wa Poland kwenye mashindano ya picha bora duniani 2023. Mashindano haya ya mchujo – yakisimamiwa na Kampuni ya Sony, hufanyika kila mwaka na mshindi huibuka na donge nono la fedha. (Picha imepatikana kutoka Forbes).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 0000448.

